Jiwe la kiroho la kujengea no. 186

## Ile mbegu ya kiroho; Wateule wa Mungu

*Wagalatia 4:6, "Na kwakuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma roho wa mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani Baba.*

Sikiliza kile Nabii wa Mungu amesema kuhusu hilo:

Mungu alipotembea juu ya maji pamoja na Nuru, na Nuru ikatokea. Ule uwepo wa kwanza wa Mungu, Nuru iliyonenwa ilikuja kwa Neno la Mungu (Mwanzo 1:3). Na Neno la Mungu ndilo pekee ambalo linaleta Nuru. Na maji yalipojitenga, zile mbegu tayari zilikuwepo duniani (Mwanzo 1:11-12) na Nuru ilichofanya ilizifanya zichipue zilezilizokuwa na chembe ya uhai, Mungu akiumba viumbe vyake.

Na sasa, asubuhi ya pasaka kuna Nuru nyingine ilikuja duniani wakati roho mtakatifu alipotolewa. Na ilitolewa kuleta Nuru kwenye mbegu zile ambazo Mungu alizijua kimbele kuwa zitakuwa hapa duniani. Kama vile alivyozijua zile mbegu za asili, Anajua zile mbegu za kiroho zilipo. Mwili wako ulikuwa uko hapa wakati huo. Mungu (kwa mara ya kwanza) alipoumba dunia. Sisi ni sehemu ya dunia. Tulikuwa tumelala pale. Na kwa ufahamu wake wa mbele alijua hasa ninani atampenda Yeye na ninani atakayemtumikia, na ambaye hatamtumikia. Ufahamu wake wa kimbele unaeleza hilo (Zaburi 139:1-18). Kama sivyo, basi yeye siyo Mungu. Hawezi akawa Mungu bila kujua yote. Na kama anajua hana kikomo Yeye anajua mambo yote (Mhubiri 3:14-15). [1].

Na leo, Mungu anawaita wateule wake, ule mzao wa kiroho wa Ibrahim kwa Imani ambayo alikuwa nayo kwenye Neno la Mungu (Galatia 3:7), unaona ule mzao wa kiroho leo ambao hauangalii kanisa la kiakili, unaona Neno. [2]

Ule uzao wa Ibrahimu haukuwa uzao wa kimwili; ulikuwa uzao wa kiroho.

Na maandiko yanasema tunapokuwa tumekufa ndani ya Kristo tunakuwa uzao wa Ibrahimu (Wagalatia 3:29). Kwa hiyo, kama umezaliwa na Roho wa Mungu (Yohana 3:3), (kama uko ndani ya YESU Kristo), wewe ni uzao wa Ibrahimu na Niwarithi pamoja na Ibrahimu kutokana na Ahadi. Na uzao wako utamiliki malango ya adui zao. [3].

Hebu tuangalie baadhi ya uzao wa Ibrahimu katika jinsi ya mwili, ambapo sisi leo ni uzao wa kiroho. Lakini hebu tutafute tujue kwa kutumia uzao wa kimwili kwa baadhi yao ambao wameamini kikamilifu ahadi ya Mungu.. [4].

Tunaweza kuangalia nyuma katika karne zote. Tunamuona Musa, Yeremia, Yohana mbatizaji, na kila mmoja wa hawa alikuwa ni mawazo ya milele ya Mungu yakidhihirishwa kwa wakati wake. Halafu tunakuja kwa Yesu Kristo ambaye ni logosi Yeye alikuwa ni wazo kamilifu na wazo lote likielelezwa na Akajulikana kama Neno (Yohana 1:1). Hivyo ndivyo Alivyo, na atakuwa hivyo milele. [5].

Wengi wenu mnaweza kuwa na ushirika na mimi katika hili wazo. Ulipokuwa kijana mdogo au msichana mdogo, utatembea hapa na pale kutakuwa na mambo fulani fulani ambayo hayakuwasumbua watoto wengine ila wewe yalikuwa, inaonekana kama kitu Fulani ndani yako kilichokuwa kinalia shauku (Zaburi 42:1-3) kulikuwa na Mungu mahali Fulani, ingawa bado ulikuwa mwenye dhambi. Unakumbuka hilo? Hakika. Sasa hiyo ilikuwa ni kitu gani? Huo ulikuwa ule Uhai mdogo uliyokuwa ndani yako wakati huo.

Na halafu baadae, ulisikia Injili. Pengine ulienda kanisani; ukaokota hiki na kile, na ukatoka dhehebu moja kwenda dhehebu lingine. Lakini siku moja, wewe ukiwa sehemu ya Mungu, unapaswa uwe sehemu ya Neno. Na uliposikia Neno, ulijua ulikotokea, ulijua ukweli ni nini, ulikuwa hivyo siku zote, ile mbegu siku zote ilikuwa ndani yako. Hivyo ilikuwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, uliliona Neno na ukalifuata hilo [6].

Angalia lile Neno haliwezi kujikana lenyewe.

Halafu sasa linatosheleza au ni ile shauku. Ni shauku ya nini? Ni kitu gani kimekuwekea hiyo shauku kwa kuanzia? Kwa sababu ndani katika nafsi, [7] Nafsi ni nini? Ni wewe, Wewe ni nafsi sehemu iliyo ndani yako [8].

Ilikuwepo mbegu iliyochaguliwa kimbele ambayo ilikuwa uzima wa milele iliyolala pale, siku zote ilikuwepo pale. "Wote aliyonipa Baba watakuja kwangu (Yohana 6:37) Hakuna hata mmoja atakayepotea".

Mtu anayefikiri akisikia Neno la Mungu, "Kondoo wangu wanaisikia sauti yangu, mgeni hawatamfuata" kwa sababu ndani pale kuna uhai, na uhai unaungana na uhai. (Yohana 10:3-4). Dhambi

inaungana na dhambi, na dhambi ni nafiki sana mpaka inafikiria imeokoka wakati haija okoka. Iko katika vilindi vya unafiki.

Wanachama wa kanisa wanataka chujio la dhehebu ili kwamba waweze kuwa na tamaa zao wenyewe na bado iwe kwenye kundi la watu wa kidini. Unawasikia wao wakisema oh yeye ni wakidini sana".[7].

Na tulipokuwa tunaenda ndani ya hii miduara juu ya zile hisi tano katika duara ya nje….. hizo ndizo ziletazo hizo hisi tano kwenye mwili. Kunanjia moja pekee uwezayo kuingia katika mwili, hiyo ni kupitia hizo hisi tano; Kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Hakuna njia nyingine ya kuwasiliana na mwili.

Ndani ya mtu yule ni mtu aitwaye Roho . Naye anazo hisi tano; Kuwazia, Hoja, Upendo, Upambanuzi, na kukumbuka (Memory). Vizuri/Vema.

Sasa, huwezi ukafikiri na mwili wako;unafikiri na akili yako. Na ndani hapo ndipo wakristo walio wengi wanaishia. Na wanaweza, kama vile tu mahindi kule shambani na majani katika shamba, wanaweza wakapakwa mafuta na Roho mtakatifu yule yule ambaye anampaka mafuta mwaminio wa halisi. Lakini ndani kule kwenye lile duara lingine, lile duara la tatu, ni nafsi; na hiyo imechaguliwa kimbele na Mungu. Hapo ndipo ile mbegu ya uhai halisi iko pale.

Lile kanisa la wakati wa Laodikia, liko uchi, kipofu, maskini, na wala halijui hilo…(Ufunuo 3:14-17). Unaona limepakwa mafuta na Roho halisi. Unaona kwamba Roho mtakatifu anaweza kuwajia watu katika roho zao, lakini ile nafsi ndio chembe ya uhai wenyewe. Ile chembe ya uhai ni Neno. Unaona? Sijali unahubiri kwa kiasi gani, jinsi unavyofanya vizuri hiki na kile, na jinsi unavyokuwa na unaupendo…… Hizo ni njia tu za mawasiliano za roho. Huwezi ukapenda na mwili wako, unapenda na roho yako. Hiyo ni moja ya njia za mawasiliano. Na unaweza ukawa na upendo na hata umpende Mungu, na bado ukawa huko sahihi. Unaweza ukatoa pepo, na kuhubiri na kufanya mambo haya, na bado uwe huko sahihi (Matayo 7:21-23). Yesu alisema hivyo; wengi watakuja katika siku ile. Na hilo Neno linamaliza hilo. [9]

Sasa inasema kuwa "Ametuchagua sisi ndani yake(Yesu) kabla ya kuwekwa misingi ya dunia"(Efeso 1:4). Hiyo inamaanisha tuko pamoja naye katika akili na mawazo ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Hilo linatupa wateule hali ya kuwa ni wa milele. Huwezi ukalikwepa hilo.

Hawa wateule siyo tu mawazo ya milele ya Mungu ambayo inabidi yadhihirishwe katika mwili kwa wakati wake, lakini hawa hawa wateule wanaitwa kwa jina lingine (Warumi 4:16)(Warumi 9:7-13) [5]

Na alipofufuka mwana wa Mungu asubuhi ya Ista(Easter), na akamtuma Roho mtakatifu (Matendo 2:1-4), ilikuwa iihuishe pia ule uzao wa Uzima wa milele, Ambao aliujua kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, ambao ungekuwa hapa. [10]

Na uzao halisi wa Mungu unanyweshwa na Roho. Mambo yote ya kidhehebu yameondolewa; kutokuamini kote kuko nje. Na Roho mtakatifu anapokuja katika chembe ile ya uhai ambayo imelala pale inazaa uzao mwingine, mwana wa Mungu mwingine anazaliwa (Amini), Mungu mwingine mdogo mwana wa Mungu. [11].

"Na kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa.."(1Korintho 12:13). Na yule Roho ni uhai wa kristo(hiyo ni sawa?), uhai wa Kristo. Na uzima wa mbegu yeyote, ambaye yeye alikuwa ni mbegu uzao wa Neno, anauleta kila uzao mbegu katika uzima. Unalipata hilo? Kama ule uzima umelala katika ile mbegu na ubatizo wa Roho mtakatifu anakuja juu yake, inalazimika kuileta ile mbegu kwenye uzima [12].

Kwa kifo chake Mungu, kule kumwagika kwa damu kume wanunua tena walio wake(1Petro 1:18-20). Amewanunua kukomboa tena Bibi Arusi wake Neno lililonenwa. "kondoo wangu wanaisikia sauti yangu(Neno) na wananifuata mimi". Siku zote ulikuwa ni kondoo. Kamwe hujawa nguruwe au mbwa aliyegeuka kuwa kondoo. Hiyo haiwezekani kwa kuwa kila mbegu huzaa kwa jinsi yake na hakuna mbegu inayobadilika (Mwanzo 1:24) [5].

Sasa Mungu katika miaka hii elfu sita alipandikiza mbegu hizi zote za ajabu au amelinena Neno lake. "Itakuwa hivi; hii miti itakuwa, Hii itakuwa hivi" (Mwanzo 1:11-12) kila kitu kilikuwa kikamilifu. Ilikuwa ni vema. Naye akaamrisha kila moja ya hizi mbegu kwamba zingekuwa. Zingejibadilisha kuwa mimea ya aina ambayo Mungu amenena ule uzima wake uwe kwa Neno alilolinena kuihusuiwe. Kama ni miti ya qak, inazaa mi ya qak, kama ni miti ya mitende itazaa mitende.

Kwa sababu yule muumbaji mkuu amelituma Neno na Neno mbegu lilikuwa pale kabla ya ile mbegu halisi haijaumbika. Na lile Nen ndilo limeumba ile mbegu unaona, Aliumba dunia kwa mambo yasiyoonekana. (Waebrania 1:3 unaona. Aliifanya dunia kwa Neno lake. Mungu alinena kila kitu ili kiweze kuumbika. [13].

Sasa kama unauzima wa milele, kama tunauzima wa milele basi siku zote tulikuwa nao, kwa sababu kunaaina moja ya uzima wa milele.

Siku zote tulikuwa. Na sababu tulikuwepo ni kuwa sisi ni sehemu ya Mungu na Mungu ndiye pekee aliye na uzima wa milele.

Sasa sisi tu sehemu ya Mungu. Siku zote ulikuwa hukumbuki hilo kwa sababu ulikuwa tu wazo la Mungu. Ulikuwa katika mawazo yake, jina lako hasa; kama liliwahi kuwa katika kitabu cha uzima, limewekwa hapo kabla ya kuwekwa misisngi ya dunia (Ufunuo 13:8). Alijua kile ulichokuwa.

Ninasema haya tu, sio kuchanganya mafundisho, lakini ni kuyanyoosha vizuri ili kwamba tuwe mbali na hofu na woga: hujui wewe ni nani: utakuja kuwa nani; lakini wewe ni mwana wa Mungu. Unaona. Siku zote ulikuwa mwana wa Mungu (Wagalatia 4:6-7). Unaona?

Kwa maana Mungu alipokuwa nawe katika mawazo yake hapo mwanzo, lazima uwe, sehemu yako Fulani, uhai\ uzima wako ambao uko ndani yako sasa. Ulikuwa pamoja na Mungu kabla ya ……vema, kabla hujawa kitu kilichoonekana hapa duniani. Kabla hakujawa na chochote, ila Mungu, ulikuwa moja ya mawazo yake. Alijua jina lako lingekuwa nani. Alijua rangi ya nywele zako ulizonazo. Alijua vyote juu ya wewe. Jambo pekee lililotokea ni ulipokuwa mwenye dhambi…… [6]

Kila mbegu itazaa kwa jinsi yake. Kama ni mbegu ya Mungu, wazo lake, mwana wa Mungu. Hapo sasa Neno la Mungu linapondwa ndani yako. Unaona? Na sasa unapolisikia Neno la Mungu,
"kondoo wangu wanaisikia sauti yangu, mgeni hawatamfuata"….. unalipata hilo? Hapo sasa kila mbegu inakuja sawa na aina yake. [14]

Katika lugha ya wazi, yule Bibi Arusi halisi wa kristo alikuwa milele katika akili za Mungu. Ingawa hawakudhihirishwa mpaka ulipokuja wakati wa kila mmoja kuja katika wakati na msimu uliopangwa. Kadiri ya kila mhusika alipokuja aliweza kudhihirishwa na kuchukuwa mahali pake katika mwili. Kwa hiyo huyu Bibi arusi ni Neno hasa lililonenwa mbegu ya Bibi arusi ingawa ni mke katika kuelelezwa yeye bado anaitwa pia "mwili wa Kristo" ni sawa hasa aitwe hivyo kwasababu yeye alikusudiwa kimbele ndani yake, walitokana na asili moja alikuwa wa milele Naye, na sasa anamdhihirisha Mungu katika viungo\watu wengi kwenye mwili ambapo wakati mmoja alidhihirishwa katika mtu mmoja, ambaye ni Bwana wetu Yesu Kristo.

Kwa hiyo sasa tunakuja kwenye hitimisho, kama vile Logosi wa milele (Mungu) alidhihirishwa katika mwana na katika Yeye ulikaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili na yule mmoja alikuwa Baba akidhihirishwa katika mwili, na kwa namna hiyo akapata jina/cheo cha mwana, na hivyo hivyo sisi, tukiwa wa milele katika mawazo yake tukawa watu wengi wa Neno lake mbegu, lililonenwa, tukidhirishwa katika mwili na mawazo yaha ya milele sasa yanadhihirishwa katika mwili na wana wengi wa Mungu, kama vile tuitwavyo. Hatukuwa uzao kwa kule kuzaliwa tulikuwa uzao kwa hiyo tunazaliwa kwa maana ni wateule tu ndio wanaozaliwa. Kwa sababu tulikuwa uzao ndio maana tunaweza kuhuishwa. Katika kile ambacho siyo uzao (mbegu) hakuna chakuhuishwa (Wagalatia 4:6)

"Nimempenda Yakobo, bali Esau nimemchukia, kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda Neno jema wala baya" (Warumi 9:13)

unaona ,ni lile wazo ,na sasa lile wazo likadhihirishwa na mungu akamkomboa yakobo ,kwa sababu yakobo pekee alikuwa ni uzao (mbegu)yakobo pekee ndiye alikuwa na uzao ,ndiyo maana alikuwa na heshima kwa ile haki ya mzaliwa wa kwanza na agano la Mungu. Kama wewe ni mbegu ya kweli ,utalisikia neno ;Roho atakubatiza katika mwili wa kristo akikujaza na kukutia nguvu wewe na utalipokea neno la wakati wako na siku yako.

[5]

Na huwezi ukawa na wazo lolote la kuwa sahihi na Mungu, mpaka kwanza yeye akuvute (Yohana 6:44). Kwa hiyo inakuja kwa kuteuliwa, si ndio hivyo? (Yohana 15:16). Na kila mmoja hapa ambaye amewahi kumsikia Mungu akibisha katika milango ya mioyo yao wanapaswa kuwa watu wenye furaha sana duniani kwa hakika. Kwa sababu kuna watu ambao kamwe hatabisha katika milango ya mioyo yao. Anaweza, lakini yeye ili awe Mungu, Anapaswa kujua mwanzo na mwisho. Hapendi yeyote apotee, unasema wewe "Mhubiri ni kwa namna gani sasa unahubiri injili? Unajuaje? Sijui ni nani. [15].

---

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk.)

---

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa: Charles E. Y. Kanju

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*